OFISI YA RAIS –TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE.
SHULE YA SEKONDARI CHARAMBE

S.L.P 104864 TEMEKE -DAR ES SALAAM

TAREHE…….

JINA LA MWANAFUNZI……..
DAR ES SALAAM

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARICHARAMBE WILAYA YA TEMEKE MKOA WA DAR ES SALAM MWAKA 2021.**

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza** katika shule hii mwaka **2020.** Shule ya sekondari ya Charambe ipo umbali wa km **12** kaskazini/mashariki/magharibi/kusini mji Mkuu wa Mkoa / Halmashauri ya manispaa ya **Temeke.**

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021.**Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **06/01/2020,** na mwisho wa kuripoti ni **ndani ya siku saba baada ya kuchukua fomu hii.**

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1Sare/mavazi rasmi ya shule

1. **WAVULANA**
   - (i) Suruali 2 (kitambaa cha shule kijani 1)
   - (ii) Shati 2 (nyeupe)
   - (iii) Viatu vya ngozi visivyochongoka mbele
   - (iv) Begi jeusi la kubebea vitabu
   - (v) Tai mbili (kijani 1)
   - (vi) Raba za michezo (wanamichezo) nyeupe siku ya ijumaa tu.
   - (vii) Soksi nyeusi na dark blue jozi 2
   - (viii) Mkanda mweusi usio na marembo
2. **WASICHANA**
   - (i) Sketi 2 (kijani 1)
   - (ii) Shati 2 (nyeupe)/ nusu kanzu mikono mirefu watakaopenda kuvaa Hijabu (kitumike kitambaa kizito cha tetron)
   - (iii) Viatu vya ngozi vyeusi visivyochongoka mbele
   - (iv) Soksi nyeupe ndefu jozi 2
   - (v) Begi la kubebea vitabu
   - (vi) Raba za michezo kwa (wanamichezo) nyeupe siku ya ijumaa tu.

2.2 Soma maagizo yafuatayo kwa makini kisha uyatekeleze.

- Jaza fomu ya kukubali kujiunga na fomu ya ahadi
- Jaza fomu za kukubali kuandikishwa.

•Fomu ya kupimwa afya (medical examination form) ijazwe katika hospitali ya Wilaya/ Mkoa/Taifa na siyo ya mtu binafsi au dispensary mfano Zakhem au Majimatitu.

3.0 MIPAKA YA SHULE

Shule ya Sekondari Charambe imezungushiwa uzio wa mabati upande wa mashariki na kaskazini. Upande wa Mashariki na kusini imepakana na makazi ya wananchi. Upande wa Magharibi imepakana na barabara ya kwenda Chulwi, na upande wa kaskazini bonde la mto.

4.0 RUHUSA YA KUTOKA NJE YA MIPAKA YA SHULE

a) Ruhusa ya kutoka nje ya shule kwa muda tu au siku inatolewa na Mwalimu wa darasa. Mwalimu wa zamu kwa pasi (kibali maalumu)
b) Ruhusa ya kutoka nje ya Dar es salaam itatolewa na Mkuu wa Shule au Makamu kwa pasi (kibali maalumu). Apatapo ruhusa ya nje ya Shuel, mwanafunzi anapaswa kuwahi kurudi
c) Ruhusa ya kwenda hospitali inapatikana kwa kupewa kibali na Mwalimu wa darasa au Mwalimu wa zamu.

5.0 MAHUDHURIO

a) Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vya masomo vya ndani na nje ya darasa kama ilivyoonesha kwenye ratiba.
b) Wanafunzi wote wanatakiwa kuhuduria na kushiriki katika shughuli zote za shule kama vile baraza la shule ukaguzi wa usafi. Kupandisha Bendera ya Taifa na kazi za mikono
c) Ni lazima kutii kengele au wito wa shughuli yoyote ya shule kwa haraka na bila kuchelewa
d) Kuhudhuria zamu za shule za mwisho wa wiki au likizo
e) Utoro wa rejareja na wa kudumu (utoro sugu) utapelekea mwanafunzi kufukuzwa shule.

6.0 MALI NA VIFAA VYA SHULE

Wanafunzi wote wanatakiwa kutunza kwa uwezo wote mali na vyombo vya shule vilivyo chini ya uangalizi wao.

a) Hakuna chombo au kifaa cha aina yoyote kinachoruhusiwa kutoka mahali pake kwa matumizi au shughuri zisizo idhinishwa
b) Iwapo chombo kimeamishwa kwa shughuli maalumu ni lazima kirudishwe mahali pake mara tu baada ya matumizi husika.
   Uharibifu au upotevu wa kifaa chochote cha Shule makusudi ama uzembe lazima ulipiwe na muhusika.

7.0 MATIBABU

a) Huduma ya kwanza itatolewa shuleni
b) Inapobidi kwenda nje ya shule kwa ajili ya matibabu ni lazima kuwa na ruhusa kutoka kwa Mwalimu wa zamu.
c) Shule haitawajibika na gharama zilizotumika / zitakazotumika kumtibu mwanafunzi katika Zahanati / Hospitali ya binafsi / Serikali nje ya Shule.

8.0 LUGHA YA MAWASILIANO

Lugha rasmi kwa maandishi au kwa kuzungumza shuleni ni Kiingereza. Hivyo tumia kiingereza wakati wote.

9.0 VITU VISIVYORUHUSIWA

1. Pete
2. Kunyoa nyusi
3. Herein
4. Kupaka rangi
5. Rangi ya kucha
6. Kucha ndefu
7. Kupaka piko (rangi nyeusi) kwenye nywele / upara
8. Kukali au kulitachi ni marufuku
9. Hairuhusiwi kunyoa mtindo
10. Hairuhusiwi kunyoa vipara
11. Hairuhusiwi kuwa na nywele ndefu au kusuka nywele
12. Hairuhusiwi kuvaa mabuti na viatu vinavyofanana na jeshi
13. Hairuhusiwi kuvaa sandozi, mikanda na vazi rasmi la shule
14. Mashati makubwa sana na slim fiti hayaruhusiwi
15. Simu ya mkononi
16. Kuja na redio shuleni
17. Kuja na game shuleni
18. Kuvaa suruali zinazobana **(modo)**
19. Kuvaa sketi zinazobana na fupi (juu ya goti) sketi ziwe chini ya goti

TAFADHALI SOMA KWA MAKIN MAELEZO / MAAGIZO HAYA NA KUTATEKEZA KIKAMILIFU

KARIBU SANA CHARAMBE SEKONDARI

.....
SHUKURU LUKAS NKOKELO
MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS –TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE.
SHULE YA SEKONDARI CHARAMBE

S.L.P 104864 TEMEKE -DAR ES SALAAM

KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Shule ni eneo linalotoa mazingira mazuri ya kumwezesha mwanafunzi kusoma na kupata elimu. Ili malengo yaliyowekwa yaweze kutimizwa hakuna budi ziwepo sheria na taratibu zitazolenga wahusika. Ni lazima wahusika wazielewe na kutii kwa kadiri inavyoelekezwa.

1. **MIPAKA YA SHULE**

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kujua eneo lote la shule na mipaka yake. Maeneo yafutayo yanahesabika pia kuwa ni nje ya mipaka ya shule:-

(i) Chumba cha walumu (staff room) na vyumba vya idara mbalimbali
(ii) Maabara ya sayansi
(iii) Ofisi za utawala na ghala zote
(iv) Jikoni
(v) Maeneo ya miradi
(vi) Nyumba za walimu
(vii) Nje ya Dar es salaam

2. **RUHUSA YA KUTOKA NJE YA MIPAKA YA SHULE AU NJE YA DAR ES SALAAM.**
   (a) Ruhusa ya kutoka nje ya shule kwa muda fulani tu wa siku inatolewa na mwalim wa zamu kwa kibali maalum.
   (b) Ruhusa ya kutoka nje ya Dar es salaam inatolewa na mkuu wa shule au makamu wake kwa kibali maalum.
   (c) Apatapo ruhusa ya nje ya shule mwanafunzi anapaswa kuwahi kurudi.
   (d) Ruhusa ya kwenda Hospitali inaanza kupewa cheti kutoka kwa Patron/Matron wa shule au mwalimu wa malezi au wa zamu.
   (e) Watoro watapewa adhabu kali na mzazi atalipa gharama za polisi jamii.
3. **NGUO RASMI ZA SHULE**
   I. **SARE YA SHULE**
      (a) Suruali kwa(wavulana) na iwe imeshonwa kwa kuzingatia maagizo ya kujiunga na shule. Ivaliwe na mkanda mweusi. Sketi kwa (wasichana) yenye mshono kulingana na maagizo ya shule .
      (b) Modo, mlegezo, vibajaji, kandambili haviruhusiwi. Hijabu ziwe pana na siketi ndefu
      (c) Shati jeupe lenye mikono mifupi. Lishindiliwe pamoja na tai ndefu
      (d) Viatu vya ngozi vyeusi kwa wavulana na vyeusi kwa wasichana na visivyo na visigino virefu na vivaliwe na soksi kufuatana na sheria za shule.

II. UVAAJI WA SARE

Sare ya shule katika mazingira yafuatayo

(a) Wakati wa masomo

(b) Mwanafunzi atokapo nje ya shule.

(c) Katika mikutano yote ya shule na mikutano ya hadhara.

(d) Chomekea shati, vaa tai muda wote na shati liwe na lebo ya shule/muhuri wa shule.

III. UNADHIFU

(a) Muda wote sare iwe safi na iliyo nyooshwa

(b) Wanafunzi wote wakate nywele ziwe fupi. Ni marufuku kuweka nywele dawa au kupaka kucha rangi.

4. MAHUDHURIO

(a) Kila mwanafunzi yampasa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo vya ndani na nje ya darasa kama ilivyoonyeshwa kwenye ratiba na kufanya kazi za darasani. Kutofanya majaribio na mitihani ni kosa kubwa.

(b) Wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria na kushiriki katika shughuli zote za shule kama vile baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa na kazi za mikono na zile watazopangiwa na mwalimu wa zamu. Ni lazima mwanafunzi akimbie afikapo “smart area”

(c) Ni lazima kutii kengele au wito wa shughuli yoyote ya shule kwa haraka na bila kuchelewa

(d) Kuhudhuria zamu za kuja mwisho wa wiki au likizo kama itakavyopangwa.

5. MALI NA VIFAA VYA SHULE

Wanafunzi wote wanatakiwa kutunza kwa uwezo wao wote mali na vyombo vya shule vilivyo chini ya uangalizi wao.

(a) Hakuna chombo au kifaa cha aina yoyote kinachoruhusiwa kutoka mahali pake kwa matumizi au shughuli ambazo hazikuidhinishwa.

(b) Iwapo chombo kimehamishwa kwa shughuli maalumu ni lazima kirudishwe mahali pake mara baada ya matumizi husika.

(c) Uharibifu na upotevu wa kifaa chochote cha shule kwa makusudi ama uzembe lazima ufidiwe na mhusika.

6. MWENENDO MWEMA WA NIDHAMU

(i) Msalimu mwalimu kwa heshima wakati wowote unapoonana naye hasa kwa mara ya kwanza kwa siku hiyo na mpokee chochote alichobeba hata mgeni anayeingia shuleni.

(ii) Mwanafunzi asimame wakati mwalimu ama mtu yeyote anayemzidi umri anapopita au kuingia darasani. Mwelekeze mgeni inapohitajika kufanya hivyo.

(iii) Usizungumze na mwalimu ama mtu yeyote anayekuzidi umri wakati mikono iko mifukoni, kiunoni, ama kofia kichwani au ukiwa umevaa miwani ya jua au kutafuna kitu mdomoni. Huo ni ukosefu wa adabu.

(iv) Usibishane na mwalimu au kiongozi yeyote bila sababu maalumu. Uamuzi wa mwalimu ni wa mwisho pamoja na hayo mwanafunzi anayo nafasi ya kujitetea na atasikilizwa.

(v) Usifanye kelele za fujo au ghasia katika sehemu zinazohitajika ukimya kama vile Ofisini, Darasani,Maabara,Maktaba na kwenye Gwaride.

(vi) Usiwe mchafu kimwili au kimavazi, uwe na nywele fupi bila kunyoa kipara, ndevu,masharubu,zinyolewe kwa wembe. Uwe nadhifu mda wote.

(vii) Jengo la utawala, eneo la bendera ni eneo la ukakamavu (smart area) ni lazima mwanafunzi akimbie anapopita eneo hilo.

(viii) Hairuhusiwi mwanafunzi kuwa na simu darasani au eneo la shule. Ukikamatwa nayo hutarudishiwa na adhabu nyingine zitafuata.

(ix) Usicheze kamali, karata wala drafti au michezo mingine isiyoruhusiwa shuleni.

(x) Timiza wajibu au kazi uliyopangiwa, fanya majaribio na mazoezi yanayotolewa darasani.

(xi) Usitumie lugha ya matusi, uhuni na mitindo isiyokubaliwa.

(xii) Onyesha heshima kwa walimu na Raia wengine wote

(xiii) Usiwe ndani au karibu ya vilabu,baa ya pombe hata kama hunywi pombe. Usivute sigara au kutumia madawa ya kulevya.

(xiv) Usiandike mahali pasipohusika kama vile kutani, vitabuni, chooni, darasani,au kwenye samani.Majina yasiyo kubalika hayaruhusiwi (nick names).

(xv) Usimpige au kumshambulia mwanafunzi mwenzako ama hata mtu mwingine yeyote.

(xvi) Usikatae uteuzi wa kushiriki shughuli mbalimbali kama vile michezo, uongozi,maandamano, uwakilishi n.k

(xvii) Usifanye biashara yeyote shuleni

(xviii) Usichelewe shule kutoka likizo na usipitishe siku za ruhusa ya kuwa nje ya shule.

(xix) Usigune wala kuzomea wakati mwalimu au kiongozi yeyote anapotoa matangazo au hotuba.

(xx) Usibandike tangazo lolote bila ya ruhusa ya mwalimu anayehusika na mada ya tangazo hilo.

(xxi) Hotuba zote lazima zionwe na mkuu wa shule kabla ya kutolewa katika hadhara yoyote shuleni.

(xxii) Usifanye mkutano bila ya ruhusa ya mwalimu anayehusika wa kukilea kikunndi kinachohusika.

(xxiii) Usihubiri dini, siasa au jambo lolote pasipokuwa na kibali cha mwalimu.

KILA WAKATI FIKIRI KWANZA KABLA YA KUNENA NA TUMIA BUSARA KABLA YA KUTENDA

7. ADHABU

(i) Adhabu inaweza kutolewa na mwalimu yeyote kwa mwanafunzi anayeonesha utomvu wa nidhamu.

(ii) Kiranja pia anaruhusiwa kutoa adhabu kulingana na kosa lililotendwa na mwanafunzi ili mradi asipige kiboko au kuzuia kuingia darasani wakati wa masomo

(iii) Kosa linapokuwa kubwa litaandikwa katika daftari la mwanafunzi na kitabu cha kumbukumbu za adhabu. Hata hivyo mkuu wa shule ataidhinisha adhabu zinazotolewa kwa mwanafunzi.

8. MAKOSA HAYA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI BILA ONYO AU BILA KUJALI TABIA YAKO YA NYUMA:-

(a) Kuiba
(b) Kufanya mapenzi
(c) Ulevi wa aina yeyote
(d) Uvutaji bangi na sigara,kutumia madawa ya kulevya au kukutwa na madawa ya kulevya kinyume na utaratibu.
(e) Kumpiga mwanafunzi, mfanyakazi au au mtu wa familia ya mwalimu au mfanyakazi
(f) Kudharau bendera ya Taifa au Wimbo wa Taifa au wimbo wa Shule au alama nyingine yoyote ya Taifa.
(g) Kuchochea mgomo wa aina yoyote au kufanya fujo ya kuhatarisha amani na usalama penye kundi la watu.
(h) Kukataa adhabu iliyotolewa na mwalimu yeyote
(i) Kutofanya mitihani ya shule au Taifa
(j) Kumnyanyasa mwanafunzi kwa sababu ya ugeni wake au jinsia yake au umbile lake au dini yake au hali yake nyingine yeyote
(k) Kukataa kutii amri ya mwalimu au mkuu wa shule
(l) Kupata mimba, au kuolewa, kufukuzwa kwa mwanafunzi ni uamuzi wa walimu wote pamoja na Bodi ya shule.

YOTE YANAWEZEKANA TIMIZA WAJIBU WAKO KWA MUJIBU WA SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE.

KARIBU SANA CHARAMBE SEKONDARI

_____

MKUU WA SHULE

KIAMBATANISHO "C"

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING

STUDENT MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by Government Medical Officer and returned to the Headmaster of Charambe Secondary School) Box 104864 DSM.

To the Medical Officer Date……

……..

……

……

RE……

Please examine the student mentioned above and comment on his/her health by responding to the following items. Kindly put a tick or cross in front of either YES or NO as you find appropriate.

…….

SHUKURU L. NKOKELO

MKUU WA SHULE

1. Does the student have problem in connect with
   a. Sight? (1) NO (2) YES
      If yes state…….
   b. Hearing? (1) NO (2) YES
      If yes state……
   c. Speech? (1) NO (2) YES
      If yes state……
   d. T.B ? (1) NO (2) YES
      If yes state……
   e. Blood Pressure? (1) NO (2) YES
      If yes state……
   f. Any physical disability (1) NO (2) YES
      If yes state……
2. Do you, therefore recommended the said student medically fit for student at this school? (1) NO (2) YES. If no please, state the reasons.
   ……..
   Date……Name& Signature of
   M.O…… Stamp……